Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili 00005809 Toleo 22: Juni 2016

Huduma Bora za Afya kwa Wote

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Singida Simon Mumbee ambaye ni mmoja wa watendaji waliotoa ushirikiano katika kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za umma.

Pongezi Wilaya Kutoa Taarifa za Umma

Na Maria Kalavo

Sikika inashukuru na kupongeza ushirikiano mzuri uliotolewa hivi karibuni na watendaji wa Serikali katika wilaya mbalimbali nchini. Pongezi hizo zinatokana na mafanikio yaliyopatikana katika zoezi la kukusanya taarifa za awali za Mpango Mkakati wa Sikika uliofanyika Aprili 2016.

Kwa namna ya kipekee, Sikika inawapongeza watendaji na wananchi wote walioshiriki katika zoezi hilo kutoka wilaya za Kinondoni, Kilwa, Kigoma Vijijini, Kasulu, Kilolo na Moshi Vijijini. Zingine ni Siha, Kondoa, Simanjiro, Singida Vijijini na Chunya. Shukrani zingine ni kwa Manispaa za Mbeya, Lindi na Temeke pamoja na Mpwawa, Musoma na Serengeti.

Katika wilaya hizo, zoezi la kukutana na watendaji kama Mganga Mkuu, watoa huduma , wajumbe wa Bodi za Afya, Madiwani na wananchi wanaotumia huduma za afya lilifanyika bila urasimu ambapo lilichukua takribani muda wa siku moja hadi tatu kwa kila wilaya.

Wakusanya taarifa walipokelewa na kupewa ushirikiano stahiki na hakuna wilaya hata moja ambapo wakusanya taarifa walitumia muda mrefu, tofauti na miaka ya nyuma.

Pamoja na pongezi hizo, shirika lingependa kuona kwamba ushirikiano huu uliooneshwa kwa Sikika unaendelezwa hadi kwa wananchi hususan wanapokwenda kutafuta taarifa ama huduma mbalimbali katika ofisi hizo.

Kupitia zoezi hili la kukusanya taarifa za awali,ilibainika kwamba wananchi bado wanapata changamoto ya kupata taarifa na kukosa huduma stahiki pale wanapozihitaji kutoka katika ofisi za umma.Pia iligundulika kwamba baadhi ya masjala bayana zilikuwa zikichelewesha taarifa kuwafikia walengwa. Sikika inapendekeza kwamba masjala bayana ziboreshwe na zitumike kama daraja la kuwaunganisha wananchi na watendaji badala ya kuwa kikwazo cha kuzuia wananchi kuwasiliana na watendaji katika ofisi za umma.

NDANI

Pongezi Wilaya kutoa Taarifa za Umma 1
Huduma za Afya Zipewe Kipaumbele 2
Tupieni Macho Zahanati ya Mpara!..... 3
Uhaba wa dawa, Watumishi bado changamoto 4

HALIUZWI

Mama na wanae wakitoka kupata chakula cha lishe na huduma ya afya katika kituo cha afya cha Ilongero, Mkoani Singida.

Huduma za Afya Zipewe Kipaumbele

Na Hendry Samky, Kigoma

Katika robo hii, Sikika ilifanya kazi ya kukusanya takwimu za awali ili kupata taarifa za kuboresha Mpango Mkakati wake wa miaka mitano, 2016 – 2020. Baadhi ya mikoa iliyotembelewa ni pamoja na Singida, Manyara na Kigoma. Katika ziara hiyo, mambo kadhaa yalijitokeza ambayo yanagusa upatikanaji wa huduma za afya.

Upatikanaji na Usimamizi wa Fedha

Katika ukusanyaji wa mapato, bado vituo vya kutolea huduma za afya havina mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato. Mfano, katika wilaya za Kigoma Ujiji na Kasulu Vijijini, hapakuwa na mashine za kupokea malipo kielektroniki. Hali hiyo inaweza kusababisha mapato mengi kupotea. Pia vituo bado havina mwongozo wa kudhibiti makusanyo na matumizi ya mapato (Health Facility Financial Management Manual).

Utawala bora na huduma za afya

Utawala bora una nafasi kubwa ya kuboresha huduma za afya katika jamii. Ni moja kati ya maeneo yanayobeba dhima ya usimamizi shirikishi wa vituo vya huduma za afya kutokana na uwepo wa Bodi za Afya za wilaya na kamati za usimamizi wa vituo vya afya. Serikali imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kuhakikisha uwepo wa vyombo hivi katika ngazi mbali mbali. Hata hivyo, changamoto iliyopo ni uelewa wa majukumu ya kamati na Bodi hizo na namna ya kuyatekeleza.

Moja kati ya mambo ambayo wadau wa sekta ya afya waliyapendekeza katika wilaya za Ikungi, Singida vijijini, Musoma Mjini, Serengeti, Kigoma Ujiji na Kasulu ni kujengea uwezo kamati hizi ili zitekeleze majukumu yake ipasavyo.

Madawa na Vifaa tiba

Changamoto ya upatikanaji wa madawa na vifaa tiba imekuwa ikisumbua vituo vingi vya huduma wilayani Serengeti na Musoma Mjini, mkoani Mara.
Mfano, kwa kipindi cha miezi zaidi ya mitatu, kuanzia Disemba 2015 kulikuwa na uhaba mkubwa wa dawa hasa 'antibiotics'.

Zahanati ya Nyakitono iliyopo wilayani Serengeti ni moja kati ya vituo vilivyo athirika sana na adha ya uhaba wa dawa kutoka bohari kuu ya dawa ya taifa licha ya kuwa na fedha za kutosha katika akaunti yao ya kituo.

Ofisi ya Mganga mkuu wa Wilaya ya Musoma ilikiri uhaba huu na kueleza kwamba unatoka na ukosefu wa dawa MSD, japo walikuwa na mkakati wa kununua dawa kwa watu binafsi baada ya kuwashirikisha viongozi wa serikali na MSD Kanda ya Ziwa. Rai ya wadau kutoka mikoa hiyo ni kuboreshwa kwa MSD ili waweze kukidhi mahitaji ya vituo. Pia, wanapendekeza mfumo wa uanzishwaji wa maduka ya MSD katika hospitali hasa za wilaya na mikoa upewe kipaumbele.

Upungufu wa Watumishi Sekta ya Afya

Idadi ya watumishi ndani ya sekta ya afya bado imekuwa changamoto ikilinganishwa na muongozo wa rasilimali watu-Afya (IKAMA 2013). Kwa sasa upungufu ni asilimia 51% kitaifa, hata hivyo, pamoja na jitihada zilizopo za kupunguza pengo hili, bado katika ngazi za wilaya hasa za pembezoni hali si nzuri. Mfano, wilaya za Serengeti (Mara), Kasulu na Kigoma, baadhi ya zahanati zina mtumishi mmoja tu, mfano, zahanati za Tamkeri na Monuna wilayani Serengeti.

Nini kifanyike kwa mujibu wa Sera na Mipango?

Dira ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa miaka mitano (2015 – 2020) inalenga kutoa huduma bora za afya kwa kila kaya nchini. Hii inaenda sanjari na kuboresha bajeti ya sekta ya afya iliyojikita katika mahitaji ya jamii. Mpango mkakati huu umelenga kuboresha maeneo muhimu ya sekta ya afya ikiwemo Rasilimali watu, madawa na vifaa tiba, rasilimali Fedha na Utawala Bora.

Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa wananchi wote wapate huduma za afya bila kikwazo cha fedha wala kujali hali yao ya kiuchumi katika jamii. Aidha, Sera imesisitiza uwepo wa vyanzo vya fedha vinavyoaminika pamoja na kuhakikisha sekta ya afya inapata rasilimali za kutosha za kugharamia huduma za afya.

Hivyo basi, ili kutoa huduma bora za afya kwa kila kaya, ni muhimu maeneo ya Madawa na vifaa tiba, rasilimali watu afya, bajeti na utawala bora yatiliwe mkazo na kupewa kipaumbele hasa katika utekeleza wa Mpango wa Matokeo Makubwa sasa (BRN) katika sekta ya afya.

Tupieni Macho Zahanati ya Mpara!

Na Atuswege Mwangomale, Kilwa

Mpara ni zahanati iliyoko katika Halmashauri ya Kilwa Masoko na ilijengwa takribani miaka 50 iliyopita. Zahanati hiyo inahudumia vijiji viwili ambavyo ni Mpara na Mpanyule. Ni zahanati inayotoa huduma za afya za nje na za uzazi kwa akinamama wajawazito.

Kwa muda wa takribani miaka 10, zahanati ya Mpara imekuwa na watumishi wa afya wawili tu kati ya watumishi kumi na tano wanaopendekezwa na ikama ya Wizara ya Afya, Wazee, Jinsia na Watoto (Staffing Level-2014-2019; MoHCDGEC). Watumishi hawa ni wahudumu wa afya ambao mmoja wao ndiye msimamizi wa kituo na wote wamepata mafunzo ya mwaka mmoja. Kwa pamoja, wanafanya kazi za ushauri, maabara, kutibu na kuwazalisha akinamama wajawazito na kusimamia kazi zote za utawala.

Uchakavu wa jengo, Vichomea takataka & maji

Jengo la zahanati hii ni chakavu na halijakarabatiwa kwa muda mrefu sasa. Paa lake nimechakaa kiasi cha kukaribia kuanguka na kuwa hifadhi ya popo. Sakafu ya jengo hili imechimbika kiasi kwamba mgonjwa au mtu yeyote anayepita lazima achukue tahadhari kwani anaweza kuanguka. Mbali na jengo la kituo kuwa chakavu, hakuna sehemu maalumu ya kuteketezea takatakana hivyo zinatupwa kwenye shimo la wazi, kitendo ambacho kinaweza kusababisha maambukizikwa wagonjwa wanaofika kupata huduma. Zaidi, kituo hakina maji kabisa, wahudumu wanawajibika kutembea takribani kilometa mbili kununua maji yanayouzwa kwa Tshs. 100 kwa ndoo.

Malipo ya ummeme

Pamoja uwepo wa umeme katika zahanati hii, mkuu wa kituo anaeleza kwamba malipo ya ankara za umeme hayana akaunti maalumu na hakuna mfumo uliopo wa kulipa na hivyo kuwalazimu kujichangisha ili kuwasaidia kupata umeme. “Kituo kinakusanya fedha za papo kwa papo wa huduma za afya.Fedha hizo zinapelekwa kwenye akaunti maalumu katika mamlaka ya mji mdogo…fedha hizo hazitumiki kulipa bili ya umeme”.Anasema Bi. Massawe na kuongeza kuwa pamoja na taarifa hii kupelekwa katika ngazi za juu bado ufumbuzi haujapatikana.

Huduma za uzazi

Wajawazito wanaofika kujifungua wanazalishwa na mhudumu wa afya, ambaye kitaaluma sio mjuzi wa kuzalisha ila anafanya kutokana na uzoefu. Bi. Massawe anasema “nimekuwa nikiifanya kazi hii kwa zaidi ya miaka kumi na namshukuru Mungu sijawahi kupata matatizo”. Bi Massawe anaeleza kwamba linapokuja suala la kujaza fomu za Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA) sehemu ya kuzalisha wajawazito inakuwa ngumu kwani inatakiwa ijazwe na mkunga aliyesomea.

Ushauri

Ili kukabilkiana na changamoto za watumishi katika sekta ya afya pamoja na nyinginezo, tunaishauri serikali na hasa halmashauri ya mji wa Kilwa Masoko kuipa kipaumbele zahanati hii kwa kuiongezea wataalamu wenye ujuzi na vile vile kuwapa mafunzo zaidi watumishi waliopo. Mazingira ya zahanati yaboreshwe kwa kufanyiwa ukarabati, kujenga sehemu ya kuteketezea takataka ili kuzuia maambukizi ya magonjwa.

Mhudumu wa afya katika kituo cha afya cha Kiganamo wilayani Kasulu akiwa amezungukwa na akinamama wanaongoja kupata huduma.

Mhudumu wa afya akiwa nje ya mlango wa kuingia kwenye makazi yake, jengo hili pia linatumika kwa huduma za maabara na huduma ya Mama, Baba na Mtoto (RCH).

Uhaba wa Dawa, Watumishi Bado Changamoto

Na Thomas Ludovick

Uhaba wa dawa, vifaa tiba na watumishi wa afya ni miongoni mwa changamoto zilizopo katika baadhi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma nchini.

Hayo yamebainika katika zoezi la tathmini ya awali lililofanywa na shirika la Sikika kwa lengo la kukusanya taarifa za awali katika sekta ya afya hususan nyanja za utawala bora, rasilimali watu katika afya, dawa na vifaa tiba na usimamizi wa fedha za umma.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wanaopata huduma katika baadhi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali wanasema kuwa changamoto kubwa ni upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na uhaba wa watumishi katika huduma za afya.

“Tatizo la ukosefu wa dawa ndio changamoto kubwa katika hospitali yetu, kila nikija kutibiwa hapa naambiwa dawa hakuna…leo nimekuja tena kupata matibabu naambiwa dawa zote nilizoandikiwa hapa hakuna, sasa inanibidi nikanunue nje kwenye duka la dawa…gharama zake ni kubwa na sijui kama nitaweza kuzimudu.” Anasema Mzee Juma Selemani katika hospitali ya Kinyonga, wilayani Kilwa.

Nae, Bi. Husna Hemmed kutoka kijiji cha Tingi, wilayani Kilwa ambaye alikwenda kupatiwa matibabu katika Kituo cha afya Tingi, amelalamikia suala la ukosefu wa dawa na kusema kuwa ni tatizo kubwa linalosababisha wagonjwa wengi kukosa dawa na kuwalazimu kununua kwenye maduka ya watu binafsi ambapo gharama zake huwa ni kubwa.

“Wagonjwa wengi wanaotoka kupatiwa matibabu hapa hawapati dawa…mimi kila nikija kupata matibabu naambiwa dawa hakuna. “Hapa kuna mchezo unafanyika,kwa sababu haiwezekani kituo kama hiki kikose dawa kila wakati lakini duka la nje la mtu binafsi liwe na dawa za kutosha… inawezekanaje?” Anahoji Bi Husna.

Mbali na suala la uhaba wa dawa pia kumekua na changamoto kubwa ya watumishi katika Idara ya afya hususan katika baadhi ya vituo vya afya na zahanati huku wananchi wanaokwenda kupatiwa huduma katika vituo hivyo wakilalamika kufika vituoni mapema na kukaa kwa muda mrefu bila kupatiwa matibabu kwa wakati.

“Nimefika hapa kituoni tangu saa kumi na mbili asubuhi, sasa hivi ni mchana ndio natoka kupatiwa matibabu…zahanati hii ni kubwa ina hudumia watu wengi kutoka maeneo mbalimbali… lakini daktari ni mmoja tu anayetoa huduma hapa.” Anasema Bi. Fatma Juma katika zahanati ya Buza, jijini Dar es Salaam.

Mganga Mfawidhi wa zahanati ya Buza, Mary Mushi anasema kuwa kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa watumishi katika idara ya afya hususan kwenye zahanati yake hali inayosababisha wagonjwakusubiri muda mrefu kwenye foleni.“Kwa mfano mimi natakiwa kuhudumia wagonjwa hapa, muda huo huo nahitajika kule kliniki kwa ajili ya kutoa huduma pia…ndio maana unaona hapa msongamano ni mkubwa kwa sababu daktari nipo peke yangu, najitahidi kujigawa ili niweze kuhudumia wagonjwa kadri niwezavyo.” Anasema Mganga huyo.

Suala la uhaba wa dawa pia ni changamoto ambapo Bi. Mushi anakiri kuwalipo na kueleza kwamba mfumo wa sasa uliopo katika Bohari Kuu ya Dawa (MSD) unastahili maboresho ili dawa zifike kwa wakati na kiasi kile kile kilichoagizwa.

Changamoto nyingine zinazohitaji kushughulikiwa ili kuboresha huduma za afya katika baadhi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali ni ukosefu wa maji na umeme, vizimba vya kuchomea takataka, masanduku ya kutolea maoni, vyumba vya faragha vya ushauri nasaha, magari ya kusafirishia wagonjwa (Ambulance), na uchakavu wa majengo.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183 - Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57
Ujumbe Mfupi: +255 688 493 882

Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua Pepe: info@sikika.co.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
@sikika1
Sikika Tanzania
sikikatanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Nukushi: 026 23 21316